East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda

Stanislas Munyengabire[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Rwanda-Koleji, S. L. P. 5039, Kigali, Rwanda.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: ipsummondele@gmail.com

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

Tarehe ya Uchapishaji:

15 Machi 2024

Istilahi Muhimu:

TEHAMA, Lugha ya Pili, Ufundishaji na Ujifunzaji, Zana za Kiteknolojia.

IKISIRI

Katika enzi hizi, TEHAMA inatazamwa kama kifaa cha kurahisisha maisha. Inarahisisha maisha kwa kuathiri kila uwanja wa maisha ya mwanadamu (Mikre, 2011). Athari hizi zinajitokeza katika shughuli zote za mtu wa kisasa. Katika uga wa elimu, ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili nao uliathiriwa sana kutokana na TEHAMA. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa makala haya kutokana na malengo mahsusi matatu. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha nne katika shule teule za sekondari nchini Rwanda. Lengo la pili lilikuwa kuchambua hasara za matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne katika shule teule za sekondari nchini Rwanda. Lengo la tatu nalo lilikuwa kubainisha namna ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, usaili, na upitiaji wa maandiko. Sampuli ilikuwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha nne katika shule teule za sekondari nchini Rwanda pamoja na wazazi wa wanafunzi hao. Sampuli ilipatikana kwa mbinu ya sampuli lengwa. Utafiti ulioibua makala haya uliongozwa na Nadharia ya Uunganisho. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba TEHAMA ni nyenzo mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu hutumiwa kufundisha msamiati, sarufi na stadi nne za lugha hasa kwa kutumia nyeno kadhaa za kiteknolojia. Aidha, utafiti huu umebaini kwamba TEHAMA inapotumiwa vibaya inaweza kusababisha madhara makubwa kwa wanafunzi. Baadhi ya madhara hayo ni pamoja na kuamini lugha ya mtandaoni zaidi, maandishi ya mkononi (kalamu) mabaya, kuathiriwa na tabia na damaduni za nje, na kutokubaliana kati ya mwalimu na wanafunzi juu ya masomo. Mwishoni, makala imejadili namna ya kuitumia TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ya pili hususan nchini Rwanda.

APA CITATION

Munyengabire, S. (2024). TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 155-169. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

CHICAGO CITATION

Munyengabire, Stanislas. 2024. "TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 155-169. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795.

HARVARD CITATION

Munyengabire, S. (2024) "TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 155-169. doi: 10.37284/jammk.7.1.1795.

IEEE CITATION

S. Munyengabire "TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 155-169, Mar. 2024.

MLA CITATION

Munyengabire, Stanislas. "TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Mar. 2024, pp. 155-169, doi:10.37284/jammk.7.1.1795.

UTANGULIZI

Katika miongo kadhaa iliyopita, ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili ulipiga hatua na kuendelezwa mara kwa mara. Maendeleo hayo mara nyingi yalitokana na kuibuka kwa mbinu nyingi mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Kila mbinu ni ya kihali na hushughulikia vya kutosha utatuzi wa maswali maalumu katika ufundishaji na ujifuzaji wa lugha ya pili kwa kipindi fulani cha wakati. Ila kwa upande mwingine, kila mbinu huwa na mapungufu pamoja na matatizo ambayo hufungulia mlango kwa mbinu mpya kuibuka (Ugwu, 2015). Hali hii inatuonesha kwamba hakuna mbinu inayojitosheleza kwa miktadha yote ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili (Richard & Rodgers, 2001).

Katika enzi za kisasa, mbinu zote za ufundishaji wa lugha ya pili husaidiwa kwa kiasi kikubwa na kipengele cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hivyo, mtaala wa kisasa ambao huegemea katika uwezo unahitaji walimu na wanafunzi wa lugha ya pili watumie zana za kiteknolojia. Baadhi ya zana hizo ni pamoja na kanda za sauti, televisheni na redio, kompyuta, kamusi za kielektroniki, barua pepe, michezo ya kidijitali, intaneti, simu ya mtandao, mikutano ya sauti na mazingira ya kiteknolojia ya ujifunzaji binafsi na ya kuona, wavuti, maktaba ya kielektroniki na kadhalika. Ahmadi na wenzake (2018) wanaona kwamba programu za kielektroniki za ufundishaji wa lugha huongeza ushirikiano chanya kwa wanafunzi na walimu na kuhamasisha ujifunzaji wa lugha kwa ujumla. Kimsingi, zana hizi zina umuhimu wa kumwezesha mwanafunzi na au mwalimu kurejea maudhui yenye matatizo mara kwa mara hadi yaeleweke kikamilifu na kuzingatiwa (Mofareh, 2019). Kutokana na zana za kiteknolojia, wanafunzi na walimu huweza kushirikiana bila mipaka ya kimuda kwani wanaweza kuendeleza masomo hata baada ya darasa.

Umuhimu mwingine ni kwamba; mosi, husaidia kuwaleta wanafunzi wa jamii mbalimbali pamoja na hivyo kurahisisha mtu kutangamana na jamii tofauti, utamaduni na lugha ya watu husika bila kwenda kwa jamii hizo. Pili, kuunda jumuiya zinazojifunza ambazo huwaleta watu pamoja kwa ajili ya kujifunza kwa pamoja na kusababisha ugunduzi na uzalishaji wa maarifa. Tatu, huwasaidia wanafunzi kuboresha msamiati wao na kuwawezesha kujua maana ya maneno katika matini wanazosoma (Chikamma & Nwaudu, 2018, Yunus, 2013). Hii inaweza kutokea wakati wanafunzi husoma makala fulani mtandaoni, wanapoangalia kamusi ya mtandaoni kwa maana ya maneno ambayo haijulikani kwao. Vipengee vingi vya kileksika pia vinaweza kujifunzwa wanapotazama video zozote zenye manukuu ya lugha husika.

Utafiti wa kuunganisha TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa ujumla ni mojawapo ya maswala yanayojadiliwa sana katika nyanja ya elimu. Yunus (2013) anaeleza kwamba watafiti na walimu wengi wanaamini kwamba TEHAMA inapotumiwa ipasavyo, ina ahadi kubwa kwa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

kuboresha ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kutengeneza fursa za wafanyakazi kama lengo kuu la mtaala wa karne ya 21. Hii ina maana kwamba utumizi mbaya wa zana za kiteknolojia huweza kusababisha hasara kadhaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Hasara hizo ni kama vile; kuwa vigumu na kushindwa kwa walimu kudhibiti darasa. Hii ni kwa sababu wanafunzi hujishughulisha na maudhui yasiyolenga ufikiaji wa malengo ya somo (kama vile kutazama filamu na nyimbo au videwo nyinginezo zisizohusu somo), inaweza kuchukua muda muhimu wa kujifunza, inaweza kutumika kupita kiasi, na pia inaweza kubadilisha uzoefu wa elimu kuwa michezo kwa wanafunzi. (Yunus, 2013, Mobi na wenzake, 2015). Yunus (khj) na Mobi na wenzake (whj) walishugulikia hasara za matumizi mabaya ya TEHAMA katika nchi zao yaani hawakushughulikia muktadha wa nchi ya Rwanda. Rwanda ni moja wapo ya nchi za Afrika Masharki zilizoweka nguvu zaidi katika TEHAMA hususan katika uga wa elimu (Mukama, 2009). Kwa hivyo, kuna haja ya kutalii athari zinazoweza kuletwa na mfumo huo kwa wanafunzi wake.

Utumiaji wa zana za kiteknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili nchini Rwanda nao unapewa kipaumbele hasa kutokana na utumizi wa mtaala unaoegemea katika uwezo ambao unatumiwa. Tangu 1998, serikali ya Rwanda ilianzisha sera mbili muhimu ambazo ni pamoja na Sera ya Uendelezaji wa TEHAMA na Sera ya Uendelezaji wa Lugha katika Mfumo wa Elimu ya Rwanda (Mukama, 2009). Mnamo 2015, Rwanda iliingiza kipengele cha TEHAMA kama moja wapo wa uwezo wa msingi uliotarajiwa kukuzwa na kuendelezwa kwa wanafunzi katika kila somo (REB, 2015). Uwizeyimana (2015) anaeleza kwamba utumizi wa zana za kiteknolojia hususani utumizi wa simu unasaidia sana katika ukuzaji wa stadi zote za lugha (stadi ya kuzungumza, kuandika, kusikiliza na kusoma) nchini Rwanda.

Utafiti uliofanywa na Mugiraneza (2021), unaona kuwa kuna changamoto kadhaa katika utumiaji wa TEHAMA katika muktadha wa elimu ya Rwanda. Changamoto hizo ni kama vile; hofu ya kutumia teknolojia kwa baadhi ya walimu na wanafunzi; ukosefu wa ujuzi muhimu kwa matumizi ya teknolojia, ukosefu wa vifaa vya kutosha vya kiteknolojia kuhusiana na idadi kubwa ya walimu na ukubwa wa darasa; ufikiaji mdogo wa mtandao; na mfiduo mdogo wa mazoea katika matumizi ya teknolojia katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji. Lakini pia, idadi kubwa ya walimu haijui fursa zilizopo katika utumiaji wa zana za kiteknolojia kwa maendeleo yao ya kitaaluma na hata kwa wanafunzi wao. Changamoto nyingine ni kwamba shule nyingi hazina umeme wala mtandao na zile zilizopewa kompyuta, walimu na wanafunzi hawazitumii katika ufundishaji na ujifunzaji (Mugiraneza, 2021). Hali hii inatuangazia kwamba Sera ya Rwanda kuhusu. Matumizi ya TEHAMA katika Elimu haijafika malengo yake. Kwa hivyo, utafiti huu ilibainisha jinsi TEHAMA inavyochangia kuendeleza elimu ya Rwanda na kulitalii changamoto za mradi wa serikali ya Rwanda kuhusu TEHAMA na elimu. Aidha, utafiti huu ulitalii namna nzuri ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda.

Malengo ya Utafiti

- Kubainisha jinsi TEHAMA inavyochangia kuendeleza elimu ya Rwanda na kulitalii changamoto za mradi wa serikali ya Rwanda kuhusu TEHAMA na elimu.
- Kutalii changamoto za mradi wa serikali ya Rwanda kuhusu TEHAMA na elimu.
- Kutalii namna nzuri ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda.

Maswali ya Utafiti

- Ni mchango upi wa TEHAMA katika uendelezaji wa Kiswahili nchini Rwanda?
- Ni changamoto zipi zilizoletwa za mradi wa serikali ya Rwanda kuhusu TEHAMA na elimu?

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

- Ni namna ipi mwafaka ya kufundisha Kiswahili sanifu kwa kutumia (TEHAMA)

METHODOLOJIA YA UTAFITI

Utafiti ulioibua makala hii ulikuwa wa kitaamuli. Shule mbili za kutwa na mbili za bweni ndizo ziliteuliwa. Koleji ya Immaculée Conception na Shule ya Sekondari ya Gikonko (Kutwa) ndizo za kutwa. Shule ya Sekondari ya SAVE na Shule ya Sekondari ya GIKONKO (Bweni) ndizo za bweni. Shule hizi zote zina michepuo ya Kiswahili na zilichaguliwa kwa sababu walimu na wanafunzi wake wanashughulikia somo la Kiswahili kama somo teule katika utafiti wetu. Utafiti huu pia ulihusisha wazazi wa wanafunzi wanaosomea katika shule zilizobainisha hapo juu.

Shule ya Sekondari Immaculée Conception SAVE ilichaguliwa kwa sababu wanafunzi wake wanaonekana kuwa wa mjini. Hivyo, inawezekana kuwa wanafunzi hawa wanaathiriana na TEHAMA katika maisha yao ya kila siku. Shule ya Sekondari ya Gikonko (Kutwa) ilichaguliwa na ukaribu wake na nchi ya Burundi. Kwa hivyo, tulihitaji kuchunguza kama kuna athari yoyote ile kwa wanafunzi inayohusiana na TEHAMA au lugha kutokana na mpaka huu. Shule ya Sekondari ya SAVE na Shule ya Sekondari ya GIKONKO (Bweni) zimechaguliwa kwa sababu ni shule za bweni lakini moja inapatikana mjini (Shule ya Sekondari ya SAVE) na nyingine iko kijijini (Shule ya Sekondari ya GIKONKO (Bweni). Kutokana na sampuli zilizochaguliwa, hatuna budi kusema kwamba zinatofautiana kijografia na kitaarifa. Kwa hivyo, wanafunzi wake wanatofautiana kimaisha, kitabia, kiteknolojia, kimawasiliano nakadhalika. Hii ilitusaidia kupata data tofauti za kutufanikisha kutimiza utafiti wetu. Wazazi nao waliteuliwa kutokana na wazo la kwamba ndio msingi wa elimu ya watoto wao. Kwa hivyo, tulikuwa tunataka kujiridisha kwamba wazazi nao wanaona mchango wa TEHAMA katika elimu ya watoto wao pamoja na kuhakikisha kwamba hata wazazi wanaweza kuona hasara za matumizi mabaya ya TEHAMA kwa watoto wao.

Kila mwalimu wa Kiswahili kutoka kila shule miongoni mwa shule ambazo zimebainishwa hapo juu, aliteuliwa. Uchaguzi wa wanafunzi 10 kwa kila shule ulitumia usampilishaji wa unasibu ambapo tuliandika karatasi zinazolingana na idadi ya wanafunzi wa darasa teule. Lakini, karatasi 10 zilikuwa zimeandikwa “NDIYO” nyingine zote “HAPANA”. Hivyo basi, wanafunzi 10 waliochagua karatasi hizo za ndiyo, ndio waliteuliwa. Mbinu hii ilitumiwa kwa kila shule. Wazazi nao walichaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji usio wa kinasibu. Mbinu iliyotumika kupata sampuli ya wanafunzi kumi kwa kila shule ndiyo iliyotumika kupata sampuli ya wazazi wanne (4) kwa kila shule.

Katika utafiti wetu, tulikusanya data kwa kutumia njia tatu ambazo ni pamoja na njia ya ushuhudiaji, njia ya usaili na njia ya uchanganuzi wa matini. Data zilichanganuliwa kwa kuegemea kiini cha malengo ya utafiti wenyewe. Mtafiti alisikiliza na kuchunguza chochote kile alichopata au kurekodi wakati wa mahojiano na ushuhudiaji. Hali hii ilimbidi mtafiti kutumia mbinu zisizo za kikompyuta zaidi lakini pia kompyuta ilitumika kuandika nukuu ambazo zilichukuliwa wakati wa kukusanya data, kompyuta pia ilitumika kuhifadhi nyaraka na rekodi mbalimbali, katika uhariri wa nyaraka mbalimbali, katika uchoraji wa picha na michoro tofauti tofauti amabayo inahusiana na utafiti pamoja na uandikaji wa ripoti ya utafiti.

Aidha, tulitumia misimbo ili kutofautisha walengwa wetu wa utafiti. Tulitumia 1 kuwakilisha shule ya kwanza, 2 kuwakilisha shule ya pili, 3 kuwakilisha shule ya 3 na 4 kuwakilisha shule ya nne. Tulitumia I kwa kuwakilisha mwanafunzi kwa ujumla, A kwa kumaanisha mwalimu kwa ujumla. Hivyo basi, 1I huwakilisha mwanafunzi kutoka shule ya kwanza na 1A kuwakilisha mwalimu wa Kiswahili kutoka shule ya kwanza vile vile. 2I huwakilisha mwanafunzi wa shule ya pili, na 2A huwakilisha mwalimu wa Kiswahili kwa shule hiyo shule hiyo ya pili. 3I huwakilisha mwanafunzi wa shule ya tatu, 2A huwakilisha mwalimu wa Kiswahili kwa shule hiyo. 4I huwakilisha mwanafunzi kutoka shule ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

nne na 4A huwakilisha mwalimu wa Kiswahili kwa shule hiyo.

NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na kufanikishwa na Nadharia ya Muunganisho. Kwa mujibu wa nadharia hii, kujifunza ni mchakato ambao hutokea katika mazingira ya kuhamisha mambo ya msingi na si chini ya udhibiti wa mtu binafsi kabisa. Maarifa hupatikana ndani ya mifumo ambayo watu hushiriki katika shughuli (Mechlova & Malcik, 2012). Msingi huu unatuelezea kuwa elimu, maarifa, na ujuzi havipatikani ndani ya mtu mmoja au mtu binafsi bali hushirikishwa ili kufanikisha malengo ya elimu. Kwa hivyo, tunaona kwamba Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni nyenzo maarufu katika usambazaji, ushirikishaji na unyonyaji wa ujuzi na maarifa hasa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Nadharia ya uunganisho inapendekeza wanafunzi washirikishiane mawazo, kaida, taarifa za jumla kwa njia zifaazo. Nadharia hii inaamini kwamba teknolojia ni sehemu kuu ya mchakato wa kujifunza na kwamba muunganisho wa mara kwa mara kati ya wanafunzi mbalimbali huwapatia fursa za kufanya uchaguzi kuhusu ujifunzaji wao. Kutokana na msingi huu tunaweza kusema kwamba nadharia ya uunganishao ni ya kisasa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba majilio ya TEHAMA katika elimu si jambo kongwe. Kwa hivyo, tunaona kwamba inaandamana na mahitaji ya elimu ya kisasa ambayo inasisitiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ufundishaji na ujifunzaji. Tunaona kwamba huu ni msingi unaohamasishia walimu na wanafunzi wa lugha ya Kiswahili hususan wa nchini Rwanda kutumia TEHAMA kama nyenzo ya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili.

Nadharia ya uunganisho ina uhusiano sana na utafiti wetu kwa ajili ya misingi yake inayosisitiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kushirikisha, kusambaza na kunyonya taarifa, ujuzi na maarifa kwa kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili, kumshauri mwalimu na mwanafunzi kutafakari, kuhakiki na kuchuja mawazo ya nje na ya mtandao kabla ya kuyatumia au kuyahakikisha kama ni ya muhimu. Kuzingatia nafasi ya mwanafunzi katika utafutaji wa habari na ujifunzaji usio na mpaka hasa hasa kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama nyenzo mwafaka katika maisha ya binadamu wa zama za sasa. Hivyo basi, nadharia ya uunganisho inatoa kielelezo cha kujifunza ambacho kinakubali mabadiliko ya kitektoniki katika jamii ambapo kujifunza si shughuli ya ndani wala kibinafsi kamwe (Mechlova & Malcik, 2012). Kwa kutumia nadharia ya uunganisho, tutafaidhika sana katika kuendeleza utafiti wetu. Hii ni kwa sababu hata nadharia yenyewe inalenga ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kuegemea matumizi ya TEHAMA.

Baadhi ya misingi ya nadharia ya uunganisho inasisitiza uhakiki wa mtu binafsi. Msisitizo huu juu ya uhakiki wa mtu binafsi, unalenga kueleza kwamba utumizi wa TEHAMA si mzuri mia kwa asilimia. Hii inatokana na ukweli kwamba isipotumiwa vyema TEHAMA inaweza kukwamisha malengo ya ufundishaji na ujifuzaji na hata kuleta madhara kwa muhusika na jamii kubwa katika maisha yake ya kawaida (Mobi, Onyenanu & C Ikwueto, 2015). Kwa hivyo, tuliitumia katika hatua za utafiti huu kama vile; uundaji wa malengo, mbinu za utafiti, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wa data.

MATOEKEO

Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili Nchini Rwanda

Katika historia ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, sarufi imefundishwa kwa njia mbalimbali (Arnell, 2012). Mtaalamu huyu anaendelea kusema kwamba, siku hizi watu wengi wanakubaliana kwamba baadhi ya sarufi huwa muhimu kwa wanafunzi wa lugha, lakini jinsi inavyopaswa kufundishwa bado ni suala lenye utata. Aidha, Shang (2007) alichunguza athari za kutumia barua pepe katika uboreshaji wa utendaji lugha katika uandishi akizingatia utata wa kisintaksia, usahihi wa kisarufi na msongamano

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

wa kileksika. Matokeo yake yalionyesha kuwa wanafunzi wanafanya uboreshaji wa uchangamano wa kisarufi na usahihi wa lugha. Faida mbili kuu za TEHAMA ni kwamba inawasaidia wanafunzi kupata udhibiti wa ujifunzaji wao wenyewe na kwamba inaweza kuwasaidia walimu kupanga na kutoa ufundishaji wa kibinafsi kwa kila mwanafunzi.

Matokeo ya utafiti wetu nayo yalionesha kwamba utumizi wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi huwa na manufaa mengi. Huyu ni mwalimu 1A ambaye anafafanua mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa sarufi ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye lugha mama ya Kinyarwanda. Anasema:

> *TEHAMA inatusaidia kuonesha matamshi bora juu ya maneno yanayosumbua wanafunzi. Hali hii inatusaidia kujenga uaminifu kati yetu na wanafunzi juu ya maudhui tunayowafundisha wanafunzi wetu. Hii ni kwa sababu tunawaunganisha na wazaliwa wa lugha ya Kiswahili nao wakaweza kusikiliza matamshi sahihi juu ya mambo fulani.*

Kutokana na mawazo ya mwalimu 1A Inaonekana kwamba vifaa vya kiteknolojia vinawasaidia walimu kuwaunganisha wanafunzi na matamshi sahihi juu ya lugha. Wanafunzi wanapenda kupata uhakika juu ya mambo wanayojifunza. Hivyo basi, ni rahisi kuwashirikisha maoni ya ulimwengu kupitia TEHAMA ili wapate uhakika juu ya mambo husika hususan sarufi. Hapa walimu wengi walieleza kwamba mara nyingi wanafunzi huwa na hamu ya kusikiliza matamshi ya Watanzania kuhusu msamiati na lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Walimu hutumia You Tube, kamusi za kwenye Google ili kuwashirikisha matamshi ya wazaliwa wa Kiswahili. Hali hii inawasaidia walimu kuaminika kwa wanafunzi wao juu ya mambo wanayowafundisha. Ushuhudiaji wetu nao ulionesha kuwa kutokana na matumizi ya TEHAMA, wanafunzi wanaweza kutangamana na walimu wengine kutoka mahali tofauti ambapo wanatumia Kiswahili sanifu. Lakini pia, TEHAMA inaweza kusaidia walimu kufundisha kuhusu lahaja za Kiswahili kwa kuegemea mifano ya matamshi ya kila lahaja kupitia TEHAMA.

Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Msamiati wa Kiswahili Nchini Rwanda

Kutokana umuhimu wa msamiati katika upataji na utendaji wa lugha ya pili, wanafunzi wengi huweka nguvu zaidi katika ujifunzaji wa msamiati. Hali hii inathibitishwa na matokeo ya utafiti wetu ambapo wanafunzi walieleza kwamba wanafanya iwezekanavyo kukariri msamiati mwingi wa Kiswahili ili waweze kuzungumza Kiswahili vizuri. Kingine ni kwamba wengi wana kamusi za kielekitroniki za Kiswahili sanifu. Aidha, Husain (2018, uk. 15) anabainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Anasema:

> *The role of the computer is assumed as the role of stimuli in language learning, and they called computer as a tool stage that helps in understanding and using language through spelling and grammar checker and editing of the program and finally it is introduced CALL which includes all steps. [Jukumu la kompyuta linachukuliwa kuwa jukumu la vichocheo katika kujifunza lugha, na waliita kompyuta kama hatua ya zana ambayo husaidia katika kuelewa na kutumia lugha kupitia kichunguza-tahajia na sarufi na kuhariri programu na mwishowe CALL ambayo inajumuisha hatua zote ililetwa*. [Tafsiri Yetu]

Ushuhudiaji ulidhihirisha kwamba wanafunzi mara nyingi huwaomba walimu kutumia projekta kwa kuwashirikisha msamiati kutoka vifungu tofauti vya habari ili wajifunze msamiati zaidi. Ila, walimu na wanafunzi wa Kiswahili hawatumii TEHAMA ipasavyo katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati wa Kiswahili. Wakati wa somo, mtafiti aliona kwamba walimu wengi wana kamusi za kielektroniki katika simu zao na wanazitumia wakati wa kuchunguza maana ya msamiati maalum. Ila, hawapendi kusisitiza wala kutumia zana zinazoshirikisha na kushughulisha wanafunzi wote.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika Kiswahili Nchini Rwanda

Enzi ya kisasa ya kidijitali inahitaji zaidi uwezo wa kusoma na kuandika (Hennessy na wenzake, 2010). Kuna aina tofauti za kusoma na kuandika ambazo huwasababisha watu kutumia TEHAMA ikiwa ni pamoja na kujua kusoma na kuandika kwa kompyuta, kusoma na kuandika kwa dijiti, hamu ya kujua kusoma na kuandika, ujuzi wa kusoma na kuandika kwa habari na teknolojia, mwingiliano wa ujuzi wa kusoma na kuandika, ujuzi wa kusoma na kuandika kwenye intaneti, ujuzi wa kusoma na kuandika maktabani, ujuzi wa kusoma na kuandika kwa vyombo vya habari au upatanishi, ujuzi wa kusoma na kuandika mambo tofauti, ujuzi wa mtandaoni, kusoma na kuandika ili kuzungumza na kuona (Raseroka, 2003, katika Hennessy na wenzake, 2010).

Kutokana na kipaumbele kilichowekwa na serikali ya Rwanda katika utumizi wa TEHAMA pamoja na mawazo ya watafiti wa hapo juu, ni dhahiri kwamba TEHAMA inaweza kuchangia kwa namna moja au nyingine katika ukuzaji wa uwezo wa kuandika hususan katika somo la Kiswahili miongoni mwa wanafunzi Wanyarwanda.

Dondoo la hapo chini ni la Mwanafunzi 4I alipoeleza mchango wa TEHAMA katika ujifunzaji wake wa stadi za kusoma na kuandika. Yeye anasema:

> *TEHAMA inatusaidia hata kuuliza habari za dharura kuhusu tahajia bora za Kiswahili kupitia zana za kielektroniki kama vile Whats App, SMS au anwani pepe. Kwa mfano: Mimi nina ndugu yangu ambaye anaishi Tanzania. Mara nyingi tunajadiliana kuhusu mambo ya Kiswahili kupitia WhatsApp. Namwuliza namna sahihi ya kuandika baadhi ya maneno. Aidha, baba yangu ananiazima sikanu ili nitumie You Tube. You Tube inanisaidia kuchuguza maandishi na matamshi yake kupitia video. Hali hii inanisaidia sana katika kukuza uwezo wangu wa kuandika na kusoma Kiswahili.*

Dondoo la mwanafunzi 4I linadhihirisha kwamba wanafunzi wanaelewa umuhimu na mchango wa TEHAMA katika ukuzaji wa umulisi wa kusoma na kuandika. Wanafunzi wanajua baadhi ya nyenzo muhimu kama vile You Tube na Whats App ambazo zinaweza kuchangia sana katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hasa hasa ukuzaji wa stadi za kusoma na kuandika.

Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kuzungumza Kiswahili Nchini Rwanda

Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha unajenga muktadha mzuri wa kuleta mageuzi na uchunguzaji wa mifano ya ufundishaji wa lugha katika enzi za kisasa (Sailun na Idayani, 2021). Kwa hivyo, walimu wanaotumia TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda watambue jukumu lao kwamba si kutoa maarifa kwa wanafunzi bali ni kuwa waelekezaji katika mchakato wa kujifunza. Hii ni kwa sababu TEHAMA huweza kutoa maarifa yote anayohitaji mwanafunzi ila si rahisi kwa mwanafunzi kuyatambua, kuyachuja, na kuyahakiki mwenyewe bila msaada wa mwalimu.

Isitoshe, Sailun na Idayani (2021) wanaeleza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hasa stadi za kuzungumza kwa kusema kwamba huwafanya wanafunzi kushiriki zaidi na kuongeza ufanisi wa ujifunzaji. Kwa hivyo, kuna faida nyingi za TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika muktadha wa Rwanda. Mosi, TEHAMA huwapa wanafunzi motisha ya kupata na kutumia lugha ya Kiswahili hususan kupitia mitandao ya kijamii. Pili, huwasaidia kutafakari juu ya kile walichojifunza na jinsi gani wamejifunza. TEHAMA huwaongezea wanafunzi kujiamini na kujimotisha kufanya kazi za shuleni kwa hamasa na furahisha. Huongeza kiwango cha kuelewa kwa walimu kuhusu athari chanya za TEHAMA, kuwapa motisha wanafunzi na kuboresha utendaji wao wa kimdomo.

Mawazo ya Sailun na Idayani (khj) yanathibitisha mchango wa TEHAMA katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, msisitizo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

ukiwekwa katika utendaji wake na utumiaji wa mdomo. Hali hii inatuelekeza moja kwa moja katika mazingira ya Rwanda ambapo mtaala tumizi unaoegemea katika uwezo husisitiza utendaji wa lugha katika maisha ya kila siku ya mwanafunzi. Hivyo basi, TEHAMA huchangia pakubwa katika uafikiaji wa malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika muktadha wa nchi ya Rwanda ambayo ni kuizungumza.

Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusikiliza Kiswahili Nchini Rwanda

Data za ushuhudiaji za utafiti wetu zilituonesha kwamba baadhi ya walimu na wanafunzi baado hawajatambua mchango na umuhimu wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza. Hii ni kwa sababu wakati wa darasani, walimu wengi walikuwa na kompyuta pamoja na projekta ila hawazitumii katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza.

Hali ya wanafunzi ya kupenda kusikiliza video za Kiswahili bila wao kukizungumza, ilitufanya kuhojiana na walimu juu ya mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wao. Mwalimu 2A alisema:

> *Mimi ninapotumia video za Kiswahili, aghalabu napanga kazi za kuzungumza zenye alama ili kuwamotisha wanafunzi kusema. Naweza kuwapatia video yenye ujumbe fulani na kuwauliza muhtasari wake kwa kuushirikisha darasa kwa njia ya mdomo. Ila, hali hii inaonekana kama kupoteza muda kwa sababu ninapowauliza wanafunzi kufanya muhtasari wa kile walichosikiliza hawaandiki chochote.*

Dondoo la mwalimu 2A linatumulikia tatizo lililomo katika matumizi ya TEHAMA wakati wa ufundishaji wa Kiswahili katika shule teule. Walimu hawajui namna ya kuitumia kwa ufanisi na hawana tekniki zinazoweza kuwasaidia kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji unaoegemea utumizi wa TEHAMA. Pamoja na hayo, kuna hasara zilizotambulika kutokana na matumizi ya TEHAMA yasiyo sahihi kwa wanafunzi na walimu wa Kiswahili.

Hasara za Matumizi Mabaya ya TEHAMA katika Ujifunzaji wa Kuandika Kiswahili

Spitzer (2014) anaeleza kwamba katika enzi za sasa uandishi wa kimkono hautiliwi maanani kutokana na maendeleo ya kiteknolojia. Naye, Carr (2011) anaongeza kwamba TEHAMA ilisababisha kuhama kutoka karatasi kwenda skrini ila, hali hii haipaswi kubadilisha namna tunavyoshughulikia ubora wa maandishi yetu. Kwake, uzoefu wa utumizi wa TEHAMA umeathiri uandishi wetu wa mkono kuwa mbaya na kukosa mvuto kwa sababu ya kupuuzwa na kutotiliwa maanani.

Wakati wa mahojiano, maoni ya watafitiwa yalithibitisha madhara kadhaa yanayotokana na matumizi mabaya ya teknolojia wakati wanapojifunza Kiswahili. Hapa chini tuna maoni ya mwalimu 4A akisema:

> *Wanafafunzi wetu wanafanya mazoezi ya kuandika Kiswahili kwa kiasi kidogo sana. Hata maneno yaliyoandikwa na mwalimu hawayaandiki vizuri. Wana ulegevu wa kuandika yaani wanataka kutumia notisi wanazopewa na mwalimu ili wazifanyie fotokopi bila kutumia kalamu. Wakati mwingine wanachapisha notisi za vitabuni kwa kuogopa kuandika na kalamu. Isitoshe, wanafunzi wa zama za sasa wana maandishi mabaya sana amabayo hayasomeki kwa sababu ya kutofanya mazoezi ya kuandika kwa kalamu na karatasi.*

Dondoo la hapo juu linatuoenesha kwamba matumizi ya TEHAMA yanaweza kuwafanya wanafunzi kuwa wavivu. Hii ni kwa sababu wanapenda kuandika kupitia kompyuta na simu kisha kuchapisha na kutunza maandishi yasiyo ya kalamu. Pia, wanapenda kuchunguza tahajia bora za Kiswahili kwenye intaneti au katika kamusi badala ya kuzifanyia kwa mikono na kalamu. Kutoakana na hali hii wanafunzi hawazingatii maneno mengi katika Kiswahili kwa ajili ya kutoyazoea. Uandishi wa karatasi au daftari na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

kalamu una jukumu kubwa la kuwazoesha wanafunzi tahajia na kuwafanya warekebishe maandishi yao. Kwa hivyo, ni njia ya mazoezi ya stadi za kuandika. Katika usaili, tuliwahi kujadili na wanafunzi pia kuhusu swala hili. Haya ni maoni ya mwanafunzi 2I. Anasema:

> *TEHAMA ilirahisisha mambo. Sisi hatupaswi kufanya kazi ngumu wakati mambo yote yanayohusiana na uandishi yamerahishishwa kupitia kompyuta, simu na uchapishaji. Mwalimu anaweza kutushirikisha karatasi zenye notisi zilizochapishwa. Ujifunzaji wa kuandika irabu na konsonanti katika shule za sekondari huweza kututia aibu. Watu wengine wakiona mazoezi ya kuandika irabu na konsonanti za Kiswahili wakati tunazipata kwenye You Tube na Google wanaweza kutucheka na kutuona kama wajinga wasiojua TEHAMA.*

Dondoo la mwanafunzi 2I linadhihirisha uzembe uliosababishwa na matumizi ya TEHAMA miongoni mwa wanafunzi. Wao hawataki kuandika madaftarini kwa ajili ya kuamini notisi zilizochapishwa. Hata wanapopewa kazi za kuandika mara nyingi wanatumia kompyuta au simu na kuchapisha. Wanafunzi hawana uhusiano na yaliyomo au maudhui ya kazi kwani uchapaji wa kompyuta hauwapi muda wa kutafakari na kujenga uhusiano kati yao na maandishi, tahajia bora au yaliyomo. Hivyo basi, kama walimu na wanafunzi wa Kiswahili wanashindwa kudhibiti utumizi wa TEHAMA ipasavyp basi, utafiti uliona kwamba kuna madhara kama yafuatayo.

Mosi, ikiwa walimu huwapatia wanafunzi notisi zilizochapishwa na kuwaruhusu kukusanya kazi zilizoandikwa kwa kompyuta au simu kila wakati basi, wanafunzi hawatajua msamiati wala kuandika maneno ya Kiswahili ipaswavyo na maandishi yao ya mikono yatakuwa mabaya. Pili, ikiwa walimu wa Kiswahili wanaamini kufundisha maandishi bora ya irabu na konsonanti za Kiswahili kupitia intaneti basi, wanafunzi wataathiriwa na mambo mengine na kutozingatia maandishi hayo.

Ni bora wanafunzi watumie vifaa ya TEHAMA ila wasisahau kujizosha kuandika kwa mikono yao kwa kutumia kalamu ili wajenge uhusiano kati yao na maandishi. Walimu wa Kiswahili nao wanapaswa kutumia mbinu zinazowafanya wanafunzi kuweka umakini katika stadi za kuandika. Njia hizo ni pamoja na kuwahamasisha kutumia kompyuta na simu bila kusahau matumizi ya kalamu na chaki, kutowashirikisha sana na notisi zilizochapishwa, kuwafundisha maandishi bora ya kila irabu na konsonanti za Kiswahili, kuwaonya kuchunguza msamiati kamusini baada ya kujaribu kuukumbuka kwa kuufanyia mazoezi ya kiakili na kimaandishi.

Hasara za Matumizi Mabaya ya TEHAMA katika Ujifunzaji wa Stadi ya Kusoma Kiswahili

Kutokana na utafiti uliofanywa na Yunus na wenzake (2013) nchini Malaysia kuhusu utumizi wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kusoma Kingereza, walimu wanaeleza kwamba wanapoleta wanafunzi katika maabara ya kompyuta, ni vigumu zaidi kuwadhibiti. Wakati mwingine wanakengeushwa kuona tovuti amabazo hazihusiani na somo. Wanafunzi wanapokuwa na kompyuta mbele yao, hutembelea tovuti nyingine na hawafanyi kazi waliopewa na walimu.

Kutokana na matokeo ya utafiti wa Yunus na wenzake (khj) ni dhahiri kwamba wanafunzi hawana uwezo wa kujidhibiti juu ya mambo mengine yanayowavutia kwenye intaneti. Hivyo basi, mwalimu anaweza kudhani kwamba wanafunzi wake wako katika hali ya kusoma kazi alizowapa wakati wanatembelea na kufurahia mambo mengine yasiyohusiana na usomaji wa kazi husika. Wakati mwingine, mwalimu anaweza kuomba mwanafunzi fulani kusoma na akasoma kama anavyoombwa. Lakini, wakati wa usomaji akili yake huwa inafikiri kuhusu habari nyingine alizokuwa anashughulikia au anatarajia kushughulikia kwenye mtandao.

Matokeo ya usaili kuhusu madhara ya utumizi mbaya wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi teule, mwanafunzi 1I alituelezea maoni yake. Anasema:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

> *Ni ukweli kwamba kwenye intaneti kuna mambo na habari nyingi za kuvutia na mara nyingi hujitokeza bila sisi kuzitafuta. Unapozibonyeza zinakuvutia na kukufanya usimfuate mwalimu. Mwanafunzi anayetaka kufuata anapata uamzi wa kutoingia katika kila aina ya habari asiyoambiwa na mwalimu kuingilia. Mara nyingi, tunajifunza kusoma Kiswahili kwa kupakuwa makala na maandiko tofauti ila hatuyasomi vizuri kutokana na ukosefu wa muda. Kwa sababu muda wetu huishia katika kucheza michezo ya mtandaoni, chati za kwenye facebook nakadhalika.*

Kutokana na dondoo la hapo juu, tunaona kwamba hatuwezi kuamini wanafunzi wetu katika utumizi wa TEHAMA wakati wa somo. Hivyo basi, mwalimu anapaswa kuwa na njia mwafaka za kufundisha stadi za kusoma kwa kutumia teknolojia. Kwa mfano; mwalimu anaweza kuzima kompyuta nyingine zote wakatumia moja ambayo inayoshirikisha habari darasa lote na kutawaliwa na mwalimu mwenyewe au mwanafunzi anapoombwa. Hali hii itawafanya wanafunzi kufuata maigizo ya mwalimu bila kuathiriwa na shughuli nyingine zisizo za muhimu.

Madhara ya Matumizi Mabaya ya TEHAMA katika Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili

Wataalamu kadhaa wakiwamo Kavitharaj (2017), Uwizeyimana (2018) and Naciri (2019) wanakubaliana kwamba TEHAMA inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji wa stadi za kuzungumza. Aidha, matokeo ya utafiti wetu yanatuonesha kwamba TEHAMA inapotumiwa vibaya, huleta hasara na madhara katika ukuzaji wa stadi za kuzungumza. Hali hii inatibitishwa na mawazo ya wanafunzi wakati wa usaili. Haya ni maoni ya mwanafunzi 4I.

> *Mara nyingi tunakabiliwa na changamoto za kuzungumza lugha ya Kiswahili sanifu kutokana na utata unaosababishwa na matumizi ya TEHEMA. Sisi tunatumia You Tube sana lakini tunakutana na matamshi ya lugha ya Kiswahili yanayotuchanganya. Tunasikia matamshi mengi yanayotofautiana na yale tuliyozoea darasani. Hali hii inatufanya kutoamini yale tunayojifunza darasani. Kwa mfano: msanii Diamond anapenda kuongeza silabi [ga] mwishoni mwa vitenzi akasema "**je, utanipendaga**?" Wakati sisi tulijifunza "je, utanipenda? Msanii huyu tena anapenda kudunisha kwa kusema "**katoto karembo**". Sisi tunasema "kijitoto kirembo". Hali hii inatutatanisha sana na kutufanya kutoongewa kwa ajili ya ukosefu wa uhakika.*

Dondoo la hapo juu linatuonesha kwamba wanafunzi wanachanganywa na matamshi pamoja na tahajia wanazozikuta kwenye mtandao ambazo mara nyingi ni tofauti na zile wanazojifunza darasani. Hali hii inatokana na ukweli kwamba mtandao unapokea kila kitu hususan lahaja tofauti za Kiswahili. Aidha, wasanii wana uhuru wao wa kukiuka kanuni na sheria za kisarufi katika kazi za utunzi wao. Hivyo basi, wanafunzi wanaweza kuathiriwa na Kiswahili kisicho sanifu kutokana na matumizi ya mtandao ambapo wanakosa uaminifu wa kuongea Kiswahili.

Hasara za Matumizi Mabaya ya TEHAMA katika Ujifunzaji wa Stadi ya Kusikiliza

Wakati wa mahojiano ilibainika kwamba wanafunzi husikia baadhi ya matamshi ya Kiswahili kama vile lahaja fulani ambayo hawajifunzi darasani. Hali hii inaweza kuwafanya kutoamini mwalimu wao kwa ajili ya upotofu wa kuamini wale wanaodaiwa kama wazaliwa wa Kiswahili. Mjadala huu ulishirikishwa hata kwa walimu wa Kiswahili ili nao watoe maoni yao juu ya swala hili. Mwalimu 2A alisema:

> *Changamoto iliyopo inatokana na kwamba wanafunzi wetu wanaamini zaidi lugha inayotumiwa na wasanii mbalimbali wa lugha ya Kiswahili. Inajulikana kwamba msanii anaweza kuboronga sarufi, kufanya utohozi kwa kuswahilisha baadhi ya maneno kutoka lugha nyingine na kuharibu sarufi kimakusudi. Hivyo basi, wanafunzi wanachua lugha ya wasanii hao kama ndiyo sanifu*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

kutokana na umaarufu wao pamoja na hoja ya kwamba ni wazaliwa wa lugha ya Kiswahili.

Kutoka na dondoo la hapo juu, ni dhahiri kwamba walimu wanakabiliwa na changamoto za kimtandao ambazo zinaibua hasara za kutoaminiwa na wanafunzi wao kutokana na matumizi mabaya ya mtandao kwa wanafunzi. Hali hii inatokana na kwamba wanafunzi huamini lugha ya kimtandao kuliko ile wanayojifunza darasani. Wanafunzi wengi hawana ukweli kwamba msanii au mtunzi ana uhuru wake wa kutofuata kanuni na sheria za kisarufi. Hivyo, anaweza kutumia lugha kama atakavyo. Isitoshe, wanafunzi hushindwa kuelewa kwamba lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi ambazo zote huweza kupatikana mtandaoni. Hivyo, wanaweza kukutana na matamshi au tahajia zisizofundishwa darasani na kuziamini kama Kiswahili sanifu. Aidha, progaramu nyingi za tafsiri mara nyingi hazitumii muundo sahihi wa kuunda sentensi pengine hazina istilahi sahihi za Kiswahili.

Namna ya Kuitumia TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili Nchini Rwanda

Vitabu vya kiada havitoshi tena, walimu wanahitaji kuvirekebisha na kuleta rasilimali ya nyongeza. Hili linaweza kufikiwa kwa kurekebisha yaliyomo (kutengeneza picha za kuonekana, kubadilisha mazungumzo), kurahisisha yaliyomo, kukagua yaliyomo (kutengeneza michezo, majaribio, maonyesho ya slaidi) na kuongezea yaliyomo na michezo ya mtandaoni, nyimbo, video, nakadhalika (Korlotyan, 2015). Walimu wa lugha wana kazi kubwa ya kuhamisha ufundishaji na ujifunzaji uliokuwa ukisisitiza utumizi wa vitabu vya kiada na kuugeuza ufundishaji na ujifunzaji unasisitizia matumizi ya TEHAMA. Hili linatokana na ukweli kwamba kutokana na shughuli nyingi za kiulimwengu, lugha inajifunzwa na kuendwa kupitia mtandao zaidi ya ana kwa ana. Hivyo basi, ni bora kutekeleza na kuboresha mikakati inayoweza kufaa katika ufundishaji wa lugha ya pili ili uga wa elimu hususan elimu ya lugha uendelee kudumu.

Chepkemoi na Wanyonyi (2017) wanaeleza kwamba nchini Kenya, matumizi ya TEHAMA katika kufundisha tamthilia na michezo mingine ya kuigiza katika Kiswahili yanaweza kuboresha utendaji wa Kiswahili katika wilaya za nchi nzima. Nchi ya Kenya ni nchi jirani na Rwanda pia nchi hizi zote zipo katika Jumuia ya Afrika Mashariki. Ila, wananchi wa Kenya wanatumia lugha ya Kiswahili kama lugha mama yao. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba TEHAMA inaweza kuchangia katika kufundisha na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Rwanda kama ilivyotumiwa kueneza uchezaji wa tamthilia nchini Kenya na kuboresha lugha ya Kiswahili miongoni mwa wananchi.

Namna ya Kuitumia Tafsiri ya Google katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili Nchini Rwanda

Google ni tovuti kwenye mtandao inayotumika kutafuta kurasa na habari za kila aina kwa kutumia programu inayoitwa " injini ya kutafuta". *Google* inatoa baadhi ya aina za Programu za wavuti 2.0 kwa elimu na mawasiliano (Downes, 2007; Miller, 2011). Hii ina maana ya kwamba walimu na wanafunzi wanaweza kutumia wavuti 2.0 kwa kufundisha na kujifunza Kiswahili. Programu kadhaa za wavuti 2.0 zimetengenezwa kwa matumizi ya wazi. Mifano ni pamoja na Wikis, DropBox, Blogs, Evernote, SkyDrive na Google Apps, na kadhalika. Programu hizi za msingi wa wavuti ni za manufaa na shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, programu hizi zote ni za kusisimua na rahisi kutumiwa na wanafunzi pamoja na walimu wao (Amin, 2020).

Tafsiri ya *Google* ni miongoni mwa programu za *Google* zilizo muhimu sana na rahisi kuzitumia katika ujifunzaji wa lugha. Wanafunzi wanaweza kutumia programu hii kwa haja ya kuongeza msamiati, kujifunza kuandika na kusoma. Tafsiri ya Google pia inazingatia namna ya kusikiliza sauti za usomaji wa mambo yaliyotafsiriwa. Hivyo, ni dhahiri kwamba programu hii inaweza kusaidia sana walimu na wanafunzi wa Kiswahi darasani na hata nje ya darasa. Wakati wa usaili, mwalimu 2A alituelezea namna anavyotumia Tafsiri ya *Google*. Anasema:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

> *Tafsiri ya Google inanisaidia sana wakati nipotaka kutafsiri mambo ya Kinyarwanda au Kingereza katika Kiswahili. Progaramu hii inanipa mwelekeo ingawa mara nyingi huweza kupotosha mtu hasa katika muundo wa sentensi za Kiswahili ambao hauhusiani na ule wa Kinyarwanda au Kingereza. Kwa kuitumia programu hii, nafungua Google, naandika Google Translate na inakuja. Kwa sababu Tafsiri ya Google huwa na lugha nyingi, nachagua lugha ambazo nataka kutumia. Lugha yenye maandishi asilia huwa kwenye upande wa kwanza na lugha yenye matokeo (tafsiri) huja kwenye upande wa pili.*

Kutokana na maelezo ya mwalimu 2A, inaonekana kwamba anatumia programu ta Tafsiri ya Google na tunapata maelezo ya namna ya kuitumia programu hii. Aidha, tunaweza kuchunguza picha ya hapo chini ili kutetea na kuunga mkono maelezo ya mwalimu wa hapo juu.



Namna ya Kuitumia You Tube katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Utafiti uliofanywa na Uwizeyimana (2018) ulithibitisha kwamba idadi kubwa ya Wanyarwanada ina simu za rununu. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa wa kujifunza lugha kwa kusaidiwa na simu kuliko nyenzo nyingine.

Matokeo kutoka ushuhudiaji yalionesha kuwa baadhi ya walimu wa Kiswahili hutumia You Tube wakati wa ufundishaji. Tuliona kwamba kwenye shule 3 mwalimu alikuwa na video za kufundishia ambazo zilipakuliwa kwenye You Tube. Wanafunzi nao walionekana kuzoea na kuvutiwa na video hizo. Aidha, walimu hawaongozi wanafunzi kutumia viungo na tovuti za kujifunzia sarufi ya Kiswahili sanifu zinazoaminika. Kwa mfano: Tovuti zinazofundisha lugha, mara nyingi huwa kwenye jukwaa la You Tube. Hata vipindi vya kwenye radio na televisheni huweka video zao kwenye You Tube kwani ndipo huweza kufikiwa na watu wengi zaidi. Hivyo basi, ni bora mwalimu awaongoze wanafunzi namna ya kuitumia You Tube. Mwalimu awambie wanafunzi kwamba mtu akimaliza kufungua programu ya You Tube anaandika kile ambacho anathamani kuona katika nafasi ya kutafiti.

Namna ya Kutumia Kamusi ya Kielektroniki katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Kamusi ya kielektroniki ni kamusi ambayo data yake iko katika mfumo wa kidijitali na inaweza kupatikana kupitia idadi ya midia tofauti. Kamusi za kielektroniki zinaweza kupatikana katika aina kadhaa, ikiwa ni pamoja na programu iliyosakinishwa kwenye kompyuta ya mkononi au kompyuta ya mezani, programu za simu, au programu za wavuti. Walimu na wanafunzi wanaweza kutumia kamusi za kielektroniki kupitia mtandao au kwa kuzisakinisha katika simu na kompyuta zao ambapo huzitumia wakati wote

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

wanapotaka bila mtandao. Kamusi za kielektroniki nazo hutumika kama Tafsiri ya Google. Wanafunzi watafitiwa wa utafiti wetu walituelezea namna wanavyotumia kamusi hizi. Huyu ni mwanafuzi 4I:

> *Wanafunzi wengi wana kamusi za kielektroniki katika simu zao au za wazazi wao. Mimi sina simu yangu lakini niliweka kamusi katika simu ya mama yangu kwa sababu haitumii sana. Ninapokuwa nyumbani nikasumbuliwa na maana ya neno la Kiswahili ninalitafuta katika lugha mbili kwani nina kamusi ya Kingereza-Kiswahili kamusi ya Kiswahili-Kinyarwanda. Kamusi hizi zinanisaidia sana kwa sababu ninajua maneno mengi katika lugha ya Kinyarwanda na Kingereza kuliko Kiswahili. Hivyo, naandika neno la Kinyarwanda au la Kingereza nikapata Kiswahili chake. Mwanfunzi wengi hawajui jambo hili la kupakua, kuweka kamusi katika simu na kuitumia katika ujifunzaji wa msamiati kama kamusi ya kaida.*

Maelezo ya mwanafunzi 4I yanaeleza kwamba ingawa yeye anajua kutumia kamusi ya kielekitroniki, baado wanafunzi wengi hawajajua kuitumia. Kamusi hii ni programu ya kimsingi katika ujifunzaji wa lugha hususan msamiati, rahisi kuitumia na ya bure. Ushuhudiaji nao ulituonesha kwamba walimu wote wa Kiswahili wana Kamusi za Kingereza-Kiswahili katika simu zao. Hali hii inatuonyesha kwamba angalau walimu na wanafunzi wanaeleza umuhimu wa kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kama somo lao kuu. Tatizo lililopo ni kwamba walimu hawasisitizi wala kuelekeza wanafunzi kuitumia kamusi ya kielekitroniki ili wawe na uwezo wa kuitumia hata baada ya darasa.

HITIMISHO

Makala haya imezungumzia, kujadili, na kuwasilisha matokeo ya utafiti ikiongozwa na malengo ya utafiti. Makala imejadili mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kuuhusisha na mazingira ya Rwanda. Makala haya pia imejadili hasara zinazoweza kusababishwa na matumizi mabaya ya TEHAMA kwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili hususan katika mazingira ya Rwanda. Aidha, tumejadili namna ambavyo baadhi ya programu za kielekitroniki zinavyoweza kutumiwa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili huhusan katika mazingira ya Rwanda. Mwishoni, tumejadili jinsi ambavyo programu zilizoshughulikiwa zinaweza kutumiwa kwa kufundisha msamiati wa Kiswahili, sarufi na stadi nne za Kiswahili ambazo ni pamoja na kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza.

MAREJELEO

Ahmadi, A., Abzari, M., Nasr Isfahani, A., & Safari, A. (2018). High-Performance, Knowledge Sharing and ICT Skills. *Human Systems Management*, *37*(3), 271-280.

Amin, E. (2020). A Review of Research into Google Apps in the Process of English Language Learning and Teaching. *Arab World English Journal (AWEJ)*, *11*(1), 399-418.

Arnell, A. (2012). The use of ICT in the Teaching of English Grammar. *Sweden: Linnaeus University, Course Code: 2EN10E. Web*, *7*, 1-29.

Carr, N. (2011). *The Shallows*: What the Internet is Doing to Our Brains. New York: W. W. Norton & Company.

Chepkemoi, N., & Wanyonyi, D. (2017). The use of ICT in teaching kiswahili play in secondary schools in Uasingishu County, Kenya. *European Scientific Journal*, 13 (25) 1857 – 7881.

Chikamma. M. A & Nwaudu. U. C. (2018). Language Teaching and Technology. *Journal of Languages and Literatures (JOLL). 3 (2) 190-198.*

Downes, S. (2007). Places to Go: Google's Search Results for Net Generation". *Innovate Journal of Online Education*, 3 (4), 1-4.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

Mikre, F. (2011). The Roles of Information Communication Technologies in Education: Review Article with Emphasis to the Computer and Internet. *Ethiopian Journal of Education and Sciences*, *6*(2), 109-126.

Hennessy, S., Onguko, B., Harrison, D., Ang'ondi, E. K., Namalefe, S., Naseem, A., & Wamakote, L. (2010). Developing the use of information and communication technology to enhance teaching and learning in East African schools: Review of the literature. *Centre for Commonwealth Education & Aga Khan University Institute for Educational Development–Eastern Africa Research Report*, *1*, 1-3.

Kavitharaj, K. (2017). ICT to enhance speaking skills. International Journal of English Language, Literature in Humanities (IJELLH), 5(9), 843-847.

Miller, M. (2011). Using Google Apps. US: Pearson Education, Inc. Publishing Limited.

Mobi, M. I., U Onyenanu, I., & C Ikwueto, O. (2015). A study of the negative influences of ICT on secondary school students in Nigeria. *American Academic & Scholarly Research Journal*, *7*(5).

Mugiraneza, J. P (2021). *Digitalization in Teaching and Education in Rwanda:* Digitalization, The Future of Work and the Teaching Profession Project, International Labour Office, Geneva, Switzerland.

Mukama, E. (2009). *Information and Communication Technology in Teacher Education:* Thinking and learning in computer-supported social practice. Linköping University, Faculty of Educational Sciences.

Naciri, H. (2019). The Use if ICT to Enhance Students' Speaking Skills. University Sultan Moulay Slimane, Beni Mellal, Morocco.

REB, (2015). *Competence-based Curriculum*: Summary of Curriculum Framework Pre-Primary to Upper Secondary 2015. WordCore Communications Limited.

Idayani, A., & Sailun, B. (2017). Roles of Integrating Information Communication Technology (ICT) in Teaching Speaking at the First Semester of English Students oF FKIP UIR. *J-SHMIC: Journal of English for Academic*, *4*(2), 12-23.

Spitzer, M. (2014). Information Technology in Education: Risks and Side Effects. *Trends in Neuroscience and Education*, 3(3-4), 81-85.

Uwizeyimana, V. (2015). An Investigation into the Contribution of Mobile-assisted Language Learning to the Acquisition of English as a Second Language in Rwanda. Stellenbosch: Stellenbosch University.

Yunus, M. M., Nordin, N., Salehi, H., Sun, C. H., & Embi, M. A. (2013). Pros and Cons of Using nICT in Teaching ESL Reading and Writing. *International Education Studies*, *6*(7), 119-130.

Ugwu, I. (2015). Language Teaching Methods: A Conceptual Approach. *Obudu Journal of Educational Studies.* 9 (1) 20-34.

Mofareh, A. (2019). The Use of Technology in English Language Teaching. *Frontiers in Education Technology* 2 (3). www.scholink.org/ojs/index.php/fet.

Mechlova, E & Malcik. M (2012). ICT in Changes of Learning Theories. Emerging eLearning Technologies & Applications (ICETA), 2012 IEEE 10th International Conference. 10.1109/ICETA.2012.6418326.

Shang, H. F. (2007). An Exploratory Study of E-mail Application on FL Writing Performance. *Computer Assisted Language Learning*, *20*(1), 79-96.

Padurean, A., & Margan, M. (2009). Foreign language teaching Via ICT. Revista de *Informatica Sociala* 7(12), 97-101.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795

Hussain, Z. (2018). The Effects of ICT-Based Learning on Students'Vocabulary Mastery in Junior High Schools in Bandung. *International Journal of Education*, *10*(2), 149-156.

Korlotyan, D. (2015). New Technologies in Learning English. Hupatikana kwenye: https://prezi.com/d4ehdwyeqla5/new-technologies-in-learning-english.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.